4. Ni maagizo gani Paulo aliyatoa alipokuwa akiagiza Huduma? 2 Timotheo 4:5.
5. Je, wafuasi Wake walipaswa kuvumilia ugumu na kukumbana na mateso? 2 Timotheo 1:8; na 2:3.
6. Ni faida ya aina gani inayoleta faraja ya kweli, na kuleta furaha na kuridhika kwa nafsi? 1 Timotheo 6:6.

**Maelezo**: Baba wa Mbinguni anatamani kwamba dunia ijazwe na furaha na amani. Alimuumba mwanadamu kwa ajili ya furaha, na anatamani kujaza mioyo ya wanadamu kwa amani na furaha ya Mbinguni.

7. Je, utajiri utaleta furaha, na tumeamriwa kuridhika na nini? 1 Timotheo 6:7, 8.
8. Ni nini uwapata matajiri, na vipi kuhusu kupenda pesa? Mistari 9 na 10.
9. Ni amri gani iliyotolewa kwa wahudumu? Tuliagizwa kuiweka kwa muda gani? Mistari 11-14.

**Maelezo**: Kutumia pesa bila sababu kwa ajili ya anasa, na kwa mambo mengi ambayo watu wanaweza kuishi bila, ni dhambi, wakati kuna watu wengi wanaoteseka kwa mahitaji ya maisha, na pia wakati kuna hitaji kubwa zaidi la kiroho. Mfuasi wa kweli aliyejitolea wa Mwokozi mwenye unyenyekevu atakuwa makini katika matumizi ya kila senti.

*******************************



**Somo la Julai 26, 2025 (Av 1, 5785)**

## KUYAWEKA MAZUNGUMZO YETU KUWA MEMA

**Somo Kuu: Yakobo Sura ya 3**
**Fungu La Kukariri: Zaburi 50:23.**

1. Jinsi gani maneno yetu ni muhimu? Mathayo 12:37.
2. Maneno yetu huja kutoka wapi? Mathayo 12:34, 35.
3. Je! Sala ya Mfalme Daudi ilikuwa nini kuhusu mawazo ya moyo wake na maneno ya kinywa chake? Zaburi 19:14.
4. Amri ya tisa inakataza nini? Kutoka 20:16.
5. Ni kwa njia gani Bwana Elohim aliwaonya wana wa Israeli kuhusu ulimi? Mambo ya Walawi 19:16.
6. Je! Maneno ya mchongezi hufananishwa na nini? Mithali 26: 21-22; 17: 9.
7. Je, ni athari gani itakayotokea kwa kukosa kueneza uvumi kwa watu wanao ugomvi? Mithali 26:20.
8. Sulemani, mtu mwenye hekima, alizungumzia nini maneno yaliyofaa (kwa hekima) yakiongewa? Mithali 25:11.
9. Je, ni tofauti gani kubwa kati ya mazungumzo kutoka midomo ambayo inayodhibitiwa na





***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Tatu
2025

Ya
Julai, Agosti, Septemba.
**(Tamuz, Av, Elul, Tishri)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

Bwana na ile ambayo haidhibitiwi? Isaya 57: 19-21.

10. Anajulikana aje yule awezaye kudhibiti ulimi wake? Yakobo 3: 2.
11. Kwa nini WaMasihi wanapaswa kuwa makini sana juu ya mazungumzo yao? Mathayo 12:36, 37.
12. Je! Bwana Elohim wetu anajua yote kuhusu maneno yetu? Zaburi 139: 4.

**Maelezo**. Kitu kimoja ambacho kinaonekana kuwa rahisi na asili kwa watu wengi kufanya ni kuzungumza kwa upumbavu. Kuna mambo mengi sana ya kusema ambayo itafurahisha watu na kuwafanya wacheke. Hii ni moja ya furaha kubwa ya watu wa kidunia, lakini WaMasihi wana furaha zaidi na zaidi kuliko hii, na haifai kwao kuwa na mazoea ya kuongea maneno kama hayo ya kipumbavu.

13. Ni pamoja na nini dhambi nyingine za msingi, mazungumzo ya kipumbavu imelinganishwa? Waefeso 5: 3, 4.

******************************



12. Ni nini ingine twafaa kuzingatia ambayo itatuongoza tuwe na kiasi? 1 Petro 4:7.

*******************************

**Somo la Septemba 6, 2025 (Elul 13, 5785)**

## KUJIKANA NA KUJITOLEA HUTUHAKIKISHIA BARAKA

**Somo Kuu: Matendo 9:1-20.**
**Fungu La Kukariri: Matendo 9:16; Warumi 12:1.**

1. Ni nini imetangazwa kuwa huduma inayofaa kwa mfuasi wa Masihi? Warumi 12:1.
2. Ni hitaji gani moja ambalo Mwokozi aliwataka wale waliotakiwa kumfuata? Marko 8:34.

**Maelezo**: Kujikana na mambo ya maisha ni moja ya masomo magumu zaidi tunayopaswa kujifunza. Watu wana mwelekeo wa kufanya wanachotaka kufanya. Ni vigumu kusulubisha mwili, na kusema "hapana" kwa mambo ambayo tunayahitaji kwa ajili ya faraja yetu, ili tuweze kuweka baadhi ya mali yetu katika kazi ya Injili. Mwokozi alisema, isipokuwa tujikane wenyewe, tuchukue msalaba wetu na kumfuata, hatuna sehemu pamoja Naye. Kujikana kunafundishwa katika Maandiko yote.

3. Je, Mtume Paulo alijikana na kuteseka kwa ajili ya kazi? Matendo 9:16.



**Somo la Julai 5, 2025 (Tamuz 9, 5785)**

## UNYENYEKEVU DHIDI YA KIBURI

**Somo Kuu: Danieli 4:19-37.**
**Fungu La Kukariri: Mithali 16:19.**

1. Je! Ni mambo gani ambayo Sulemani alisema yatatokea kutokana na kiburi? Mithali 11:2; 13:10.
2. Je, kiburi na unyenyekevu vinalinganishwaje? Mithali 29:23.
3. Daudi alisema nini kuhusu kiburi? Zaburi 10:2; 12:3,4; 73:3-6.
4. Je! Ni nini kilimpata Farao kwa sababu ya kiburi chake? Kutoka 5:2; 14:8,28.
5. Kiburi kilimfanya Mfalme Uzia afanye nini, na matokeo ya mwisho yalikuwa yapi? 2 Mambo ya Nyakati 26:16, 19, 21.
6. Kwa nini ghadhabu ilitangazwa juu ya Israeli wakati wa utawala wa Hezekia? 2 Mambo ya Nyakati 32:24-26.
7. Je! Yahshua alifundisha somo gani la unyenyekevu? Luka 14:7-11.
8. Je! Paulo alitoa wito gani wa unyenyekevu? Warumi 12:3; 11:18-21.
9. Nabii Isaya alisema Mtakatifu atakaa na nani? Isaya 57:15.



7. Wakati Petro alikuwa amefungwa kwa minyororo miwili gerezani, jinsi gani alifanywa kuwa huru? Matendo ya Mitume 12:7-10.
8. Ni kupitia kwa maombi ya nani yeye alipata kusaidiwa?. Mstari wa 5.
9. Jinsi gani inawezekana kwa haraka kwake Mwenyezi Elohim kusikia maombi yetu, na kuyajibu? Danieli 9:21.

**Maelezo**: Malaika huitwa kwa msaada wetu wakati tunapoomba. Maombi ni kiungo kinachotuunganisha ambacho kinatupea nguvu takatifu za uweza ambazo ni lazima tuwe nazo ili tuishi maisha ya ushindi.

10. Ni uhusiano gani muhimu upo kati ya mtu na malaika, unaohusu uelewaji wa maandiko? Danieli 9:22.
11. Katika maumivu makuu ya Gethsemane, jinsi gani Baba wa Mbinguni alipeana msaada wa wake katika saa hii ya shida? Luka 22:43.
12. Jinsi gani tutapata msaada wa kiroho? Mathayo 7:7, 8.
13. Malaika wa Mbinguni wana nia katika masuala ya binadamu? Luka 15:10.
14. Katika wakati mkubwa wa taabu ni nani atakuwa mlinzi wetu? Zaburi 91:9, 10, 11

*******************************

**Somo la Agosti 30, 2025 (Elul 6, 5785)**

## KIASI

**Somo Kuu: 1 Petro 4.**
**Fungu La Kukariri: 1 Petro 4:7**

1. Ni kwa kiasi gani mwenye hekima alijaribu raha za dunia? Mhubiri 2:10.
2. Ni kiasi gani njia hiyo iliweza kumudu starehe ya kweli? Mhubiri 2:11; Mithali 14:12-13.
3. Ni nani hufurahishwa na starehe kama hii? Mithali 15:21.
4. Mwenye hekima alifikia hitimisho gani? Mhubiri 2:13, 14.
5. Kwa nini kuwa na kiasi hupendekezwa kuliko utovu? Mhubiri 7:2, 3.
6. Nini kinachotofautisha kati ya wenye busara na wale wapumbavu? Mhubiri 7:4.
7. Ni nini mtu mwenye hekima alimwamuru kijana kuwa makini hata katika harakati za raha? Mhubiri 11:9.
8. Ni tahadhari gani ya kuwa na kiasi imetolewa: Tito 2:2-8; Warumi 13:13; 1 Petro 1:13?
9. Je, hii inamaanisha kwamba watu wa Elohim lazima wawe wamehuzunika wakati wote? Zaburi 100:2; Isaya 12:2-3; Luka 6; 22, 23.
10. Jinsi gani MMasihi anafaa kufurahi? Wafilipi 4:4.
11. Kwa nini umakini na kuwa na kiasi ni muhimu hasa? 1 Petro 5:8.



**Somo la Agosti 2, 2025 (Av 8, 5785)**

## KULALAMIKA NA KUNUNG'UNIKA

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 10:1-11.**
**Fungu La Kukariri: Wafilipi 2:14, 15.**

1. Baada ya Elohim kuwakomboa Wana wa Israeli kwa njia ya ajabu kutoka kwa Wamisri na kuwavusha Bahari ya Shamu, walifanya nini? Hesabu 14:2-4.
2. Je, waliridhika na kile Elohim aliwapa kula? Hesabu 11:4-6.
3. Je, Elohim alifurahishwa na manung'uniko yao? Aliwaadhibu vipi? Hesabu 11:1.
4. Ni adhabu gani nyingine ya kutisha iliyoletwa kwa Wana wa Israeli kwa sababu ya dhambi hii? Hesabu 14:26-30.
5. Ni wanaume wangapi wa Wana wa Israeli waliotoka nchi ya Misri? Kutoka 12:37.

**Maelezo**: Kulikuwa na wanaume laki sita wa Israeli walipotoka nchi ya Misri. Kutoka kwa idadi hii kubwa, ni wawili tu waliokuwa na umri wa zaidi ya miaka 20 waliyoruhusiwa kuingia katika Nchi ya Ahadi. Wengine wote walikufa jangwani. Hivyo tunaona adhabu ya kutisha waliyopokea kwa kutotii.



maendeleo katika kiroho, na wakati mwingine tunaweza kukosa kupiga hatua mbele; lakini kumbuka, kwa yote, jua au mvua, Elohim ni msaada wetu wa kila wakati. Hatuwezi kukosea ikiwa tutakuwa wanyenyekevu mbele zake, na kuendelea kuomba na kuwa na hamu sana ya utakatifu.

*******************************

**Somo la Septemba 27, 2025 (Tishri 5, 5786)**

## UUMBAJI WA JUU

**Somo Kuu: Waebrania 1.**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 1:14.**

1. Ni uumbaji upi wa viumbe ambao ni sawa na mwanadamu, hali yetu ikilinganishwa na wao ni ipi? Zaburi 8:3-5.
2. Kusudi lao na ofisi katika uumbaji lilikuwa lipi? Zaburi 34: 7; Waebrania 1:13, 14.
3. Je, Muumba analo fikira kuwa mwanadamu ni wa familia moja kama malaika? Waefeso 3:14, 15; Ufunuo22:8, 9.
4. Je, familia hii ina jina sawa na ni jina gani? 1 Wakorintho 15:9; 1 Wathesalonike 2:14.
5. Ni nini imesemwa kuhusu malaika wa Mbinguni kuhusu amri? Zaburi 103: 20.
6. Ni kwa njia gani wajumbe hawa wa Mbinguni huitwa kwa msaada wetu? Mathayo 26:53.



10. Ni nini wanadamu wenye dhambi wanapaswa kufanya ili wawe wana wa Elohim? Mathayo 18:3,4; Yakobo 4:10.
11. Ni kitendo gani cha unyenyekevu ambacho Yahshua alionyesha kabla ya kusulubiwa kwake? Yohana 13:3-5.
12. Ni adhabu gani kali iliyotolewa kwa Mfalme Herode kwa sababu hakumpa Elohim utukufu? Matendo 12:21-23.
13. Je! Ni ushauri gani Yahshua anawapa wale wanaojivuna? Ufunuo 3:17,18.

**Maelezo**: Imesemwa: "Ulimi hutuingiza matatizoni na kiburi hutufanya tubaki hapo." Hilo lisidumu kwa wana wa Elohim. Na tuyakumbuke daima maneno ya Sulemani: "Pamoja na wanyenyekevu kuna hekima." Mithali 11:2.

*******************************

**Somo la Julai 12, 2025 (Tamuz 16, 5785)**

## UNYENYEKEVU WA WAAMINIO

**Somo Kuu: Mathayo 18:1-20.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 18:3.**

1. Alipokuja duniani, Yahshua aliweka mfano gani? Luka 2:11, 12 na 16.

6. Je, ni sawa kwa watu kulalamika na kunung'unika kuhusu hali za maisha leo? 1 Wakorintho 10:10.
7. Wakati akizungumzia Israeli, waliolalamika na kunung'unika, Paulo analeta jambo gani muhimu akilini mwetu? 1 Wakorintho 10:6, 11.
8. Ni maagizo gani zaidi ambayo Paulo anatoa na ni kwa nini? Wafilipi 2:14, 15.

**Maelezo**: Kulalamika na kunung'unika hakuna nafasi katika maisha ya MMasihi.

9. Hali ya maisha yetu ya kila siku inapaswa kuwa vipi kila wakati? Waebrania 13:5; 1 Timotheo 6:8.
10. Ikiwa tunaye Bwana kama mwongozaji wetu, hali ya mioyo yetu itakuwa vipi? Zaburi 16:8, 9.
11. Ni habari za aina gani tutakazokuwa tukieneza kwa wengine? Isaya 52:7.
12. Je, tutabeba msalaba kwa furaha, na kujikana wenyewe katika kazi ya Bwana? Luka 9:23-25.

*******************************

**Somo la Agosti 9, 2025 (Av 15, 5785)**

## UCHONGEZI NA KUONGEA UOVU

Hakuna mtu anapenda kusengenywa, wala hakuna mtu yeyote hufurahia kusingiziwa. Hata hivyo ni hakika hakuna uhaba wa wambeya au wasingiziaji. Hii inaonyesha kwamba wengi hawana



4. Je, mtu anapaswa kuua ili awe na hatia ya mauaji? 1 Yohana 3:15.
5. Wayahudi walijazwa na nini walipoona umati ukienda kumsikiliza Paulo akihubiri kuhusu Masihi Yahshua? Matendo 13:44-48.
6. Je! Baadhi ya matunda ya wivu ni nini? Yakobo 3:16.
7. Jinsi gani Ayubu anavyoeleza kuhusu wivu? Ayubu 5:2.
8. "Moyo safi ni uzima ya mwili". Wivu ni nini? Mithali 14:30.
9. Je, inawezekana kwa mtu kuwa katika hali ya kuokolewa na wakati huo huo kuwa na wivu moyoni mwake? Wagalatia 5:21.
10. Mtume Paulo alisema ni nini inapaswa kuondolewa ili tuwe wafuasi wa Masihi Yahshua Bwana wetu? Waefeso 4:31.
11. Hili linawezaje kutimizwa? Mstari 32.
12. Ikiwa tutafanya hivi, tutaitanishwa na kanisa gani? Waefeso 5:27.

**Maelezo**: Wivu na chuki ni dhambi na huonekana kwa sababu ya ukosefu wa Roho Mtakatifu. Ikiwa tutashinda dhambi hizi, lazima tutafute nguvu za Bwana — "Kwa maana mtapokea nguvu baada ya Roho Mtakatifu kuja juu yenu." Tunaweza kufanya mambo yote kupitia Yahshua Masihi, ambaye anatupa nguvu.

*******************************



2. Je! Ni utimilifu gani wa unabii tunaoupata kuhusu unyenyekevu wake? Zekaria 9:9; Mathayo 21:1-11.
3. Je! Yahshua alijinyenyekeza hadi kufikia kiwango gani kingine? Wafilipi 2:5-8.
4. Je! Wanafunzi walitaka kujua nini kutoka kwa Yahshua? Mathayo 18:1.
5. Je! Aliweka nani kama mfano kwao? Mathayo 18:2-4.
6. Jinsi gani Paulo anatafsiri zaidi maana ya kuwa watoto? 1 Wakorintho 14:20.
7. Sifa ya "kuwa watoto katika uovu" itatuongoza kufanya nini? Mathayo 5:43-45.
8. Ikiwa sisi ni "watoto katika uovu," tutaongozwa kufikia ukamilifu wa kiwango gani? Mathayo 5:46-48.
9. Je! Yahshua alisema msamaha wetu unategemea nini? Mathayo 6:14, 15.
10. Unyenyekevu wetu unapaswa kutuongoza kusamehe waliotukosea mara ngapi? Mathayo 18:21, 22.

*******************************



3. Ni mambo gani mawili ambayo yana sehemu muhimu katika uongofu? Matendo 20:21.
4. Tunapotimiza mahitaji haya, Elohim anaahidi nini? Matendo 3:19.
5. Paulo anatumia mfano gani akielezea kuhusu kuacha dhambi? Warumi 6: 1-7.
6. Ni nini tunafaa kufanya baada ya toba na uongofu? Warumi 6: 4.

**Maelezo**. Paulo alikuwa na tukio bora la kubadilika. Mabadiliko kamili yalifanyika katika maisha yake wakati alipofanywa kutambua kosa la mwenendo wake. Badala ya kumtesa Masihi na wafuasi wake kama alivyofanya zamani, alianza kuhubiri ujumbe wa Injili kwa nguvu nyingi mno.

7. Agano la Kale linaelezea kuhusu uongofu? Ezekieli 18:30, 31.
8. Je, Agano la Kale linasema tunapaswa kufanya nini katika uongofu? Isaya 55: 6, 7.
9. Je, Agano Jipya linasema nini kuhusu maisha haya mapya? 2 Wakorintho 5:17; Wakolosai 3: 1-10.
10. Baada ya kubatizwa, tumeambiwa tufanye nini? 2 Petro 3:18; 1 Yohana 1: 7.

**Maelezo**. - UMasihi ni tukio la siku kwa siku, tukio la hatua kwa hatua. Wakati mwingine tunaweza kuwa na mafanikio mazuri ya

8. Ikiwa watu watatupinga kwa kufundisha Kweli, je, tutawachukia kwa ukosefu wa wema? Mstari 25.
9. Ni katika nguvu za nani watu kama hao wanatangazwa kuwa? Mstari 26.
10. Je, tunapaswa kamwe kusema mabaya juu ya mtu yeyote, au tunapaswa kuonyesha upole na unyenyekevu? Tito 3:2 na 3.
11. Baada ya upendo wa Bwana kuja, ni mabadiliko gani yanayopaswa kufanywa katika maisha yetu? Tito 3:3 na 4.
12. Ikilinganishwa na ulimwengu unaodai kuwa wa KiMasihi, je, kunapaswa kuwa na tofauti yoyote kati yao na washiriki wa mwili wa Masihi, na ni kwa njia gani? Tito 2:14.

*******************************

**Somo la Agosti 23, 2025 (Av 29, 5785)**

## WIVU NA CHUKI

**Somo Kuu: Mithali 27.**
**Fungu La Kukariri: Mithali 27:2.**

1. Sulemani alisema nini katika mithali yake kuhusu wivu? Mithali 27:4.
2. Je! Wivu ni mkatili kiasi gani? Wimbo wa Sulemani 8:6.
3. Je! Matokeo ya wivu wa Kaini yalikuwa gani? 1 Yohana 3:12.



chuki halisi kwa ajili ya michezo yenyewe, na kwamba ni wakati tu wao wenyewe huwa malengo ya mishale yake ya uchungu wao ufahamu kikamilifu unyarafu wake. Wakati mwingine tunajikuta tukishiriki katika aina yoyote ya "kuzungumza mabaya" au uvumi usio na huruma, tunafaa kufanya vizuri kuchunguza nia zetu. Tungefaa pia kufanya vizuri tujiulize kama sisi kweli tunajua nini tunazungumzia. Mara nyingi watu hurudia mambo ambayo hawana ukweli dhabiti. Wanaweza hata kutojua mtu ambaye wanasingizia, lakini wamesikia tu "hili na lile" kutoka kwa baadhi ya "mwandani wake." Mwandani huyu mara nyingi, katika hali halisi, ni "mgeni" – ni kwa sababu hii yeye uanza kusingizia! Kwa hakika, baadhi ya nia kuu za kusingizia ni hisia za kujiona duni na wivu, ambao uletwa juu ya hali dhaifu ya kiroho na haja ya kuhalalisha mtu binafsi kwa kusingizia wengine.

**Somo Kuu: Waefeso sura ya 4.**
**Fungu La Kukariri: Waefeso 4:29.**

1. Ni nini chanzo cha kusingizia? Mathayo 15:19; Luka 6:45.
2. Je, tunafaa kuwaamini wale ambao ujiingiza katika kusingizia? Yeremia 9:8.
3. Nini kundi lipi la watu hufurahia kusengenya? Mithali 11: 9; Zaburi 50:20; Yeremia 6:28.



7. Katika uzoefu huu, alipata jibu saa ngapi? Mistari 20-23.
8. Je! Danieli alikuwa katika kufunga na kuomboleza kwa muda gani ili kuelewa maono? Danieli 10:2 na 3.
9. Je! Malaika alipewa agizo mapema kiasi gani ili kwenda kwake? Mstari 12.
10. Ni nani aliyemzuia malaika? Alipataje ukombozi? Mstari 13.

**Maelezo**: Tunapaswa kujifunza kuomba kama Danieli. Aliendelea kukiendea kiti cha neema hadi akapata jibu. Hakujua ni nani aliyezuia maombi yake, lakini alikuwa na imani kwamba Elohim alikuwa amemsikia, kwa hivyo aliendelea na vita hadi aliposhinda. Mikaeli (Mkuu, Danieli 10:21; 1 Wathesalonike 4:18) alikwenda kumsaidia malaika na atakuja kutusaidia vivyo hivyo (Danieli 12:1).

*******************************

**Somo la Septemba 20, 2025 (Elul 27, 5785)**

## KUONGOKA KUNAMANISHA NINI

**Somo Kuu: Wakolosai 3: 1-17.**
**Fungu La Kukariri: Matendo 3:19.**

1. Yahshua alizungumza jinsi gani kuhusu uongofu? Mathayo 18: 3.
2. Kwa nini uongofu ni muhimu? Warumi 8: 6, 7.



**Somo la Julai 19, 2025 (Tamuz 23, 5785)**

## JIHADHARI NA UGOMVI NA UDANGANYIFU

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 3.**
**Fungu La Kukariri: Warumi 16:17.**

1. Je, kuna hatari yoyote ya kudanganywa? Wakolosai 2:8; 1 Yohana 4:1.
2. Ni nini kitakachowapata wale wanaofuata mafundisho ya wanadamu? Wakolosai 2:20-22.
3. Je, wanafunzi walielewa injili au ujumbe wa Masihi mwanzoni? Luka 9:51-56.
4. Hata baada ya Pentekoste, jinsi gani Petro alishindwa katika kuongoza kanisa? Wagalatia 2:11-13.
5. Ni kwa njia gani watu hudanganyika kwa urahisi? 2 Petro 2:1-3.
6. Ni hali gani isiyofaa iliyokua Korintho ambayo inaweza kuwa ilitokana na udanganyifu? 1 Wakorintho 1:11-13.
7. Ni nini baadhi ya waongofu walijaribu kuleta kanisani wakati wa Paulo? Wagalatia 4:8-11; Matendo 15:5.
8. Paulo alipinga mafundisho haya kwa maneno gani ya nguvu? Matendo 15:10.
9. Ni mwenendo gani wa sasa uliozuia hata kanisa la kwanza? 2 Yohana 9, 10.

4. Ni athari gani za kusingizia? Mithali 6:19.16: 28, 18: 8, 26:20.
5. Mwisho wa umbeya unaoudhi, maongezi yenye ladha, maneno yaliyotiwa chumvi na uvumi ni nini? Mhubiri 10:12-14.
6. Je, sisi tutahalalishwa tukiongea maneno mabaya kwa watu fulani ambao tunadhani wanastahili hayo maneno? Tito 3:2-8.
7. Je, tutahitajika kutoa hesabu ya maneno yetu yote ambayo si ya kweli na yenye kudhuru? Mathayo 12:36,37.
8. Je, watu wanaonekana wachaji Elohim, wakati mwingine uanguka katika dhambi ya kusingizia na kuzungumza mabaya? Yakobo 1:26.
9. Ni kuhitimu kupi kunaohitajika kwa wale ambao Bwana ataruhusu ndani ya hema lake? Zaburi 15:1-3.

*******************************

**Somo la Agosti 16, 2025 (Av 22, 5785)**

## MIGOGORO NA KUSENGENYANA

**Somo Kuu: 2 Timotheo 2.**
**Fungu La Kukariri: 2 Timotheo 2:24.**

1. Je! Ni agizo gani muhimu ambalo Mwokozi anayaagiza makanisa kukumbuka? 2 Timotheo 2:14.
2. Je! Anatuonya nini kuhusu matokeo ya migogoro juu ya mambo madogo? Mstari 16.



3. Ikiwa tunafanya mambo haya yaliyokatazwa, anayalinganisha na nini? Mstari 17.

   **Maelezo**: Kidonda cha mdomo ni jeraha la kusumbua ambalo hatimaye litaharibu maisha, na kwa njia hiyo hiyo migogoro na ugomvi utasababisha kifo cha maisha yetu ya kiroho, na kusababisha kutojali na kuvunjika moyo.
4. Ni maswali ya aina gani tumeagizwa kuyazuia na ni kwa nini? Mstari 23.

   **Maelezo**: Masomo ya Biblia ambayo hayajawekwa wazi katika maandiko na yanayoweza kusababisha mabishano yanapaswa kuepukwa darasani, lakini yajadiliwe kwa faragha, kwa sababu wajibu wetu na kazi yetu ni kulisha wana-kondoo na kondoo. Yohana 21:15-17. Migogoro na mabishano hayana chakula cha afya, na mambo kama haya yanadhuru maisha ya wanyonge na watoto wachanga wa imani.
5. Je, tunapaswa kuzingatia mambo yanayoleta maswali yasiyo na maana au yale yanayojenga kwa njia ya imani? 1 Timotheo 1:4.
6. Je! Tukiwa watumishi wa Baba wa Mbinguni, ni nini anatuamuru tusifanye? 2 Timotheo 2:24.
7. Tunapaswa kuwa vipi kwa watu wote? Mstari 24.



10. Jinsi gani Yohana aliwaonya WaMasihi kuhusu wadanganyifu katika siku zake? 2 Yohana 6, 7.
11. MMasihi atalazimika kufanya nini ili kujua ukweli na kukosa kudanganywa? 1 Yohana 4:1.

    **Maelezo**: Wale wanaodanganywa kwa hiari yao wanaweza kugawanywa katika makundi mawili. Kuna wale wanaopenda maagizo ya wanadamu hivyo vizuri kwamba huwa wanakataa kukubali ushahidi kutoka kwenye Biblia — neno takatifu la Elohim linaweza kuvuruga mawazo yao sasa. Pia kuna wale ambao hawana nia ya kutosha katika ukweli ili kujifunza wenyewe.
12. Jinsi gani Yahshua alitoa onyo kuhusu wadanganyifu katika siku hizi za mwisho? Mathayo 24:4, 5, 11, 24.
13. Jinsi gani tunapaswa kuzijaribu roho? Isaya 8:20.
14. Ni juu ya msingi gani tutalazimika kujenga ili tuwe na hakika ya kutodanganywa? Waefeso 2:20-22 Wagalatia 1:8; 2 Wakorintho 13:1; Warumi 3:4.
15. Baadhi ya wachungaji wataonyesha kutokuwa na hiari kiasi gani ya kukubali ukweli wa neno la Elohim takatifu? Ezekieli 22:26-31.

*******************************



**Somo la Septemba 13, 2025 (Elul 20, 5785)**

## MAOMBI YA KILA SIKU KATIKA MAISHA

**Somo Kuu: Wakolosai 3.**
**Fungu La Kukariri: Wakolosai 3:16.**

1. Ni jambo gani muhimu ambalo lilikuwa katika maisha ya Daudi? Mara ngapi? Zaburi 55:17.
2. Kama Daudi, ni nini kinapaswa kuwa cha kwanza katika mpango wetu wa kila siku? Zaburi 88:13; 119:147.

   **Maelezo**: Neno la Kiingereza la kale lililotafsiriwa hapa "kuzuia" linamaanisha "kwenda kabla." Kwa hivyo, katika kuanza siku, maombi yetu yanapaswa kwenda mbele ya Bwana asubuhi na mapema, kabla ya shughuli zozote kuanza, hivyo kuweka mwendo wa maisha ya kila siku yenye ushindi.
3. Ni nani mwingine aliye mfano wetu kwa maombi ya mara tatu kila siku? Danieli 6:10.
4. Ni ushindi gani uliomjia kutokana na mpango huu? Mistari 21-23.
5. Ni nani mwingine aliye mfano wetu wa kuomba? Luka 6:12.
6. Ni nini kingine kinapaswa kuhusishwa na kuomba? Danieli 9:2 na 3.